



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI

(RITA)

TANGAZO KWA WANAOFUNGISHA NDOA KATIKA MADHEHEBU YA DINI

Taarifa inatolewa kwa wafungisha ndoa wa madhehebu ya dini (according to Religious Rites) kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa sura 29 marejeo ya 2002 kifungu cha 30 kinawataka kuwa na Leseni hai wanapofungisha ndoa. Ikumbukwe kuwa muda wa uhai wa Leseni ya kufungisha ndoa ni miaka mitatu na baada ya hapo inatakiwa kuhuishwa.

Hivyo, viongozi wa dini wasio na Leseni wanakumbushwa kujisajili ili wapate leseni za kufungisha ndoa na kwa wale ambao Leseni zao zimekwisha muda wanatakiwa kuzihuisha ili waweze kutimiza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria. Wakala hautasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya yeyote atakayebainika kukiuka sheria hii.

Huduma za kutoa na kuhuisha Leseni zinatolewa katika Ofisi za Makao Makuu ya RITA, Jengo la RITA eneo la Posta Mpya, Jijini Dar es Salaam. Kwa walio nje ya Mkoa wa Dar es Salaam wanaweza kupitisha maombi yao ya leseni katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Wilaya zilizopo katika kila Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Kwa Maelezo zaidi fika kitengo cha Ndoa, ghorofa ya pili, Jengo la RITA Makao Makuu au Piga simu (bila Malipo) namba 0800117482. Pia unaweza kutembelea tovuti ya Wakala www.rita.go.tz

Emmy K. Hudson

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu/ Msajili Mkuu wa Ndoa na Talaka